



Sifa ya udhu

Atanuia udhu kwa moyo wake kisha atasema bismillah kisha ataosha viganja vyake.





1

Kisha atachukua maji kwa kiganja chake cha kulia na atasukutua na kupandisha maji puani na kuyameka na ataweka kidole gumba na cha ishara puani.





2

Kisha ataosha uso wake kutokea maoteo ya kawaida ya nywele za kichwa mpaka mwisho wa taya mbili na kidevu kwa urefu na upana baina ya maskio mawili.





3

Kisha ataosha mikono yake kutokea ncha za vidole mpaka katika viwiko atanza mkono wa kulia kisha kushoto.




4

Kisha atapatangusa kichwa chake chote atapitisha mikono yake kutokea mwanzo wa kichwa mpaka kisogoni kisha atarejesha mwanzo wa kichwa.





5

Kisha ataingiza kidole chake cha ishara katika tundu za maskio yake na atapakaa kwa kidole gumba nje ya masikio.



6




Kisha ataosha miguu yake pamoja na fundo mbili.



7

- Hukumu ya kuzidisha juu ya kiwango kilichoekewa sheria ?

Haifai kuzidisha juu ya kiwango kilichoekewa sheria katika udhu kama kuzidisha kuosha mara tatu au kuosha juu ya kiwiko au juu ya fundo za miguu (miundi) au kupaka shingo.



8

- Na atasema baada ya kumaliza kutia udhu :

Ash hadu alla ilaaha illa Allaah wahdahu laa shariika lahu wa ash hadu anna muhammadan 'abduhu wa rasuluh na katika mapokezi ya tirmidhi Allaahumma j'alnii mina ttawwaabiin waj'alnii minal mutatwahririin

9

- Miongoni mwa vitenguzi vya udhu :

- 1- Chenye kutoka tupu ya mbele na nyuma kama mkojo au haja kubwa au upepo.
- 2- Kutokwa na akili kwa kulala au kuzimia.
- 3- Kula nyama ya ngamia.





10

Sifa ya tayammum

Tayammum ni badali ya twahara ya maji itakaposhindikana kutumia maji katika viungo vya twahara au baadhi yake kwa sababu ya kukosekana maji au kuhofia madhara kwa kutumia maji, basi ytachkua mchanga nafasi ya maji



1

Atanuia tayammum kwa moyo wake kisha atasema bismillah kisha atapiga pigo moja juu ya ardhi na atapangusa kwa viganja vyake uso wake na nje ya viganja vyake.



2

wala si sheria kuchanua vidole wakati wa kupiga juu ya mchanga wala kuesua vidole wakati wa kupangusa viganja viwili



3

Sifa ya josho la wajib

Atanuia kuoga kwa moyo wake na atasema bismillah Kwa siri kisha ataeneza mwili wote kwa maji na sehemu zilizo chini ya nywele chache na nyingi pamoja na kuskutua na kupandisha maji puani.

1

- Yenye kuwajibisha kuoga :

- 1- Janaba: inakuwa kwa kutoa manii kwa kuingilia au jambo jengine au kukutana kwa tupu mbili.
- 2- kutoka damu ya hedhi na nifasi.
- 3- Kifo cha asiekuwa shahiid
- 4- Kusilimu kwa kafiri

2



Ameweka taaliki **Sheikh Dukuur Haytham Sarhaan**, Mwalim wa zamani masjid annabawiy
Na msimamizi wa maahad ya sunna : mahadusunnah.com

Haki za kuchapa na kusambaza zipo huru.
Tarjama ya kipeperushi «sarhaan.com» Au pangusa bar code